

# Mapishi ya Ugali - Mtamu :-)

## LENGO/MATOKEO:

Kupika Ugali kwa ajili ya watu 4-5

## VIUNGO:

- Vikombe 2 vya unga wa mahindi
- Vikombe 4 au zaidi vya maji
- Chumvi  $\frac{1}{2}$  kijiko cha chai

## MAELEKEZO/HATUA:

- 1 **Ongeza vikombe 4 vya maji katika sufuria kubwa nzito. Ongeza chumvi  $\frac{1}{2}$  kijiko cha chai.** Chemsha hadi itokote, chota kikombe kimoja kisha uweke kando.
- 2 **Koroga taratibu vikombe 2 vya unga wa mahindi,** hadi kila kitu kiishie kwenye sufuria, ukiweka kidogo kidogo na kuendelea kukoroga kwa mwiko ili kusiwe na mabonge yoyote. Eua sufuria kwenye moto huku ukijaribu kuondoa mabonge ili mchanganyiko huo usiungue.
- 3 Punguza moto uwe kiasi cha chini kisha upike mchanganyiko huo hadi uwe mzito.
- 4 Kisha ongeza maji yaliyotokota, upunguze moto, funika na **upike kwa dakika 10.** Zima moto. Pakua vidonge kwa bakuli dogo — tingisha na utengeneze kidonge kwa kulizungusha bakuli.
- 5 Chakula sasa kiko tayari kupewa walaji!

**Chanzo:** Maudhui haya yanahifadhiwa na Meta na hivi sasa yanajumuisha mafunzo yaliyotolewa kwa shirika la Youth and Media katika Kituo cha Berkman Klein cha Intaneti na Jamii katika Chuo Kikuu cha Harvard chini ya leseni ya Kimataifa ya Creative Commons Attribution-ShareAlike 4.0. Unaweza kuyatumia maudhui hayo, ikiwa ni pamoja na kuyanakili na kuandaa kazi zinazotokana na maudhui hayo, kwa madhumuni ya kibiashara au la, ilimradi utataja mradi wa Youth and Media kama chanzo cha asili na kufuata masharti mengine ya leseni hiyo, kushirikisha kazi zingine zozote za ziada chini ya masharti hayo.